

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**  
ISO 9001:2015 CERTIFIED



## **TAARIFA KWA UMMA**

### **KUSITISHA ZUIO KWA WATOA HUDUMA KUWATUMIA “FREELANCERS” KATIKA USAJILI WA LAINI ZA SIMU**

Ikumbukwe kuwa tarehe 16 Februari, 2021 baada ya kuwa na kikao na watoa huduma za Mawasiliano ya simu, TCRA iliwaelekeza watoa huduma kusitisha kuwatumia “Freelancers” katika usajili wa laini za simu kibayometria ifikapo 1 Mei, 2021 na badala yake usajili ufanyike katika maduka au mahali maalum kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa laini za Simu za 2020.

Napenda kuwajulisha kuwa TCRA imeondoa zuio hilo kwa watoa huduma na wanaweza kuendelea kuwatumia “Freelancers” bila kuathiri usajili sahihi wa laini za simu kibayometria wakati inafanya tathmini upya ya namna bora inayoweza kutumiwa na watoa huduma kuwasimamia “Freelancers”. TCRA, inatoa rai kwa “Freelancers” kuhakikisha kuwa wanatumia weledi katika kufanya kazi yao ya usajili wa laini za simu.

TCRA itaendelea kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu huduma za mawasiliano kwa ustawi na maendeleo ya Taifa.

IMETOLEWA NA

**DKT. JABIRI K. BAKARI**  
**MKURUGENZI MKUU**  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**  
**Tarehe 14 Aprili, 2021**